KWA JINA LA ALLAAH, MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 10, Issue 4

24th Jumâ dal-Aakhir 1432

27th May, 2011

NJIA SWAHEEH YA KUPAMBANA NA MARADHI YA MAJINI

Dr. Abu'l-Mundhir Khaleel ibn Ibraheem Ameen

YALIYOMO

NJIA SWAHEEH YA KUPAMBANA NA MARADHI 1 - 4

1. KUWA NA NIA NJEMA KATIKA KUJIFUNZA NA KUFANYA KWA AJILI YA ALLAAH PEKE YAKE

Twabibu wa dawa ya Qur'an ni lazima awe muangalifu sana kuhakikisha kuwa nia yake yakuijua ilmu hii si kwa sababu ya kutaka kupata manufaa ya kilimwengu. Abu Dawood na Ibn Maajah (رحمهم الله) wamepokea kuwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) alisema: Mtume (صلي الله عليه وسلم) amesema: **"Yeyote atakayejifunza 'ilmu yoyote naiwe ni kwa ajili ya Allaah peke yake, na anayejifunza ili apate manufaa ya kilimwengu, basi hatonusa (kuisikia harufu) manukato ya Jannah siku ya kufufuliwa".** [**swaheeh-hadeeth no. 6159 swaheeh al-Jaami' al-Albaani**]

2 'ILMU

Ilmu ni sampuli mbili: 'ilmu ya Ki-islamu miongoni mwake ikiwa ni 'ilmu ya Tawheed, na 'ilmu ya kujua ni kipi halaal na haraam ili mtu asiingie katika giza la uzushi (Bid'ah); na 'ilmu ya kidunia kama 'ilmu ya watu na mazingira yao. Yule anayetaka kumtibu mwenzake ni lazima awe na 'ilmu sampuli hizi mbili.

3 UJUZI

Ni lazima vilevile awe na ujuzi wa utwabibu. Miongoni mwake ni kuwa na 'ilmu ya Majini na Mashetani na njia zao, 'ilmu ya kupambana nao, na 'ilmu ya mafungamano baina ya mgonjwa na Allaah.

4 KUWA MCHA MUNGU

Atakayekuwatibu wenziwe ni lazima awe mjuzi na awe na taqwa, ndani na nje awe mtu mwema. Ni lazima awe daima ni mwenye kutenda vitendo vyema vya ibada vyenye kumuudhi shaytaan na kumshinda nguvu.

5 KUHIFADHI SIRI ZA WATU

Ni lazima awe ni mtu awezae kuhifadhi siri, kwa sababu mambo haya yatakufanya uyajue mambo ya siri ya watu na yalio ya siri zaidi.

JIPATIE NAKALA YA KITABU CHA SWALA:

Namba za simu: 0721473181 AU 0727341779

6 KUIJUA 'ILMU YA MAGONJWA WA AKILI

Magonjwa ya akili yafanana na magonjwa yanayosababishwa na kupagawa na shaytaan, ki sampuli zote, na baadhi ya watu hutatizika na magonjwa ya ki-akili na yale yanayosababishwa na jinni au warogi.

7 UGONJWA HUCHUNGUZWA NA KUBAINISHWA VIPI?

Kwa kesi ya ugonjwa anaoupata mwanadamu kutoka kwa jinni, kama kesi yoyote ya madhara ya kiafia (medical disorder), ni muhimu kutabiri shida ugundue ni kipi kilichosababisha. Pindi twabibu ajuapo sababu ya jinni ya kumdhuru mtu yule, basi aweza kumtibu kulingana na hiyo sababu. Ikiwa ameathiriwa na mrogi, atatoa dawa yakupambana na urogi. Ikiwa ugonjwa umesababishwa na jicho ovu, atatumia dawa inayoambatana na hilo. Katika kila hali atatumia dawa ifaayo.

Ili kutabiri sababu hizo, ni lazima atayarishe mahali pa kutibu, kuondosha kila kitu mahali hapo chenye kuhusiana na kumu'asi Allaah (سبحانه وتعالى). Kwa hivyo kama kuna picha zilizoangikwa kwenye kuta au makabati na sehemu nyingine ni lazima ziondoshwe, na kama kuna ala za mziki pia ziondoshwe. Kisha atamtayarisha mgonjwa ki-mawazo kwa matibabu, kwa kumnaswihi kwa mukhtasari, na kama mgonjwa ni mwanamke ni lazima anasihiwe kuvaa hijaab na mahram zake wawepo.

Ujuzi wa twabibu ni muhimu mno katika kumtibu mgonjwa, na hayo hufanywa kwa kumfanyia mgonjwa utafiti, yuko karibu vipi na Allaah, na kumuuliza masuali mengine. Kulinga na

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

sampuli ya ugonjwa unaomuathiri mgonjwa, masuali yake huwa ni tofauti kwa kila mgonjwa. Masuali yanayoulizwa mume ni tafauti na yale anayoulizwa mke; na kwa namna hiyo hiyo yale anayoulizwa aliyefunga ndoa ni tafauti na ya ambaye bado hajafunga ndoa, na yale ya mzee ni tofauti na ya kijana.

Masuali hutafautiana kulingana na hali na aina ya ugonjwa au madhara yaliyomsibu mtu, lakini kuna masuali yanayomuhusu kila mtu ambayo twabibu huenda akahitaji kuyauliza.

*aina ya ugonjwa au madhara au shida anayo hisi mgonjwa. *lini ugonjwa au shida ilipoanza. *namna ya ndoto anazo zihisi. Kulingana na sampuli za ndoto, twabibu huweza akafahamu chanzo cha shida - ikiwa ni kitendo cha kulipa kisasi-kesi ya mapenzi au matatizo aliyoyasababisha mrogi (mchawi). *ikiwa mgonjwa ahisi kama hawezi kumkumbuka Allaah (dhikr), kusoma Qur'an au kuisikiliza Qur'an au kama ajihisi na usingizi au maruwe-ruwe (aina ya ulevi) * kama asikia uchungu ukipita ndani ya mwili, au tumboni mwake, au kufa-ganzi (**numbness in his extremities**). *ajihisi kama ataka kulia bila sababu. *kama ajihisi kubanwa katika kifua chake. *kama aumwa na kichwa daima kusichopata nafuu kwa madawa tafauti. *na je ikiwa kuna hali isiyokuwa ya kawaida kwa wanawake walio katika ada zao za mwezi (haidh)?

Haya ni baadhi ya masuali ya ki-Ujumla ambayo twabibu aweza kuuliza ili yamuezeshe kujua iwapo shida ya mgonjwa ilisababishwa na mrogi, au ni madhara yaliosababishwa na jinni, au si zaidi ya kupagawa au ni magonjwa ya ki-akili na jinni hahusiki nayo shida hiyo?

Baada ya masuali haya, twabibu afikia katika moja ya maamuzi mawili.

1– Aweza kujua sababu za shida kwa upesi.

2– Au atatatizwa kuhusu hayo.

Ikiwa twabibu atajua matatizo ni nini aweza kutibu maradhi kwa njia ifaayo. Ikiwa jinni ndio sababu basi aweza kusoma Ruqya kutoka kwa Qur'an. Ikiwa tatizo ni kurogwa basi aweza kusoma Ruqya kutoka kwa aya za Qur'an ambazo za kusanya Ruqya dhidi ya urogi au mgonjwa mwenyewe aweza kujisomea kinachotakikaniwa. Ikiwa twabibu amechanganyikiwa basi ni lazima afanye yafuatayo.

KUSOMA RUQYA: Twabibu na asome Ruqya kwa mgonjwa. Twabibu daraja yake ya Taqwa na ukaribu wake kwa Allaah una natija muhimu sana katika kumuathiri jinni ambaye anasababisha madhara. Katika kitabu chake *"Masaa'ib Al-Insaan Min Makaa'id Al-Shaytaan",* Ibn al-Muflih Al-Hanbali amesema kuwa Shaytaan hupata kifafa anapoukurubia moyo uliojaa imaan kama kifafa anachopata Binadamu. Akasema "Moyo mzima uliojaa Imaan ni nuru (muangaza), wenye moto, na wasiwasi (shaytaan mwenye kushawishi) akiukurubia , hugeuka jivu. Imesemekana kuwa ikiwa dhikr ya Allaah imetulia kisawasawa ndani ya moyo wa mtu, Shaytaan akiukurubia hupata kifafa kama kile anachopata Binadamu anapokurubiwa na shaytaan. Kisha mashaytaan hukusanyika wakimzingira na kusema "ana nini huyu?" Wakijibizana ''Binadamu amemshinda nguvu."

Jambo ni kuwa nguvu ya Imaan ya msomaji ina athari ya kumdhuru Shaytaan. Silaha ni nzuri ikiwa itatumiwa na mwenye ujuzi nayo. Aya za kusomwa ni kama zifutazo:

1. Surat al-Alfatiha

2. **Aya tano za kwanza za Al-Baqarah (1-5)**

3. **Al-Baqarah (163-164)**

4. **Al-Baqarah (255-257)**

5. **Al-Baqara (285-286)**

6. **Aali-Imraan (18-19)**

7. **Al- Araaf (54-56)**

8.**Al-Muminoon (115-118)**

9. **Al-Saaffat (1-10)**

10. **Al-Ahqaaf (29-32)**

11. **Al-Rahmaan (33-36)**

12. **Al-Hashr (21-24)**

13. **Al-Jinn (1-9)**

14. **Al-Humazah**

15.**Ikhlaas**

16. **Al-Falaq**

17. **An-Naas.**

Baada ya kusoma Ruqya huwezekana kukapatikana matokeo matatu:

1- Mgonjwa atapata kifafa **(seizure)** na jinni atazungumza, kwa hali hii basi na aulizwe kuhusu:

i. Jina lake.

ii. Dini yake.

iii. Na sababu ya kumuingia mtu huyo.

2– Mgonjwa hatapata kifafa, lakini baadhi ya dalili zitajitokeza ambazo zitakazo onyesha kuwa matatizo yamesababishwa na Jinni.

3-Hakuna vituko vitakavyotokea vyenye kuonyesha kuwa ni ugonjwa au maradhi ya ki-akili.

Ikiwa sababu ya kuingiwa na Jinni ni vitendo viovu ambavyo Allaah (سبحانه وتعالى) amevikataza, yeye (jinni) na aambiwe kuwa hili ni haraam, na ushahidi udhihirishwe dhidi yake. Aambiwe kuwa yeye yuko chini ya hukmu ya Allaah na Mtume wake (صلي الله عليه وسلم), Ambaye Allaah (سبحانه وتعالى) alimtuma kwa jamii zote mbili; wanaadamu na Majinni.

Ikiwa Jinni amefanya hivyo ili amuadhibu mwanadamu au kumlipa kisasi naye basi naambiwe kuwa mtu huyu hakujuwa alichokifanya, na yule ambaye hana nia ya kumdhuru mtu

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

kwa kukusudia hastahiki kuadhibiwa. Ikiwa wamefanya hivyo katika milki yake au nyumbani kwake basi wajulishwe kuwa nyumba hiyo ni ya binadamu na ana haki ya kufanya yanayoruhusiwa atakavyo nyumbani kwake; wewe huna ruhusa ya kukaa kwake bila ya idhni yake. Twabibu na asisitize kuwaambia wao kuhusu hukmu ya Allaah na Mtume wake (صلي الله عليه وسلم) na kuleta ushahidi dhidi yao, kuwaamrisha mema na kuwakataza maovu kama atakavyowafanyia binaadamu. Allaah (سبحانه وتعالى) akasema: **"... Na Sisi si wenye kuwaadhibisha (viumbe) mpaka tuwapelekee Mtume (awafahamishe yalio ya haki, basi wakiyakataa ndipo wanapoangamizwa."** [Al-Israa'17: 15]

"Na acheni dhambi zilizo dhahiri na zilizofichikana. Hakika wale wanaochuma dhambi watalipwa yale waliokuwa wakiyachuma." [Al -An'aam 6:120]

Ndipo Mtume (صلي الله عليه وسلم) akakataza kuwaua nyoka wapatikaniwao majumbani mpaka waambiwe kuondoka mara tatu, kama ilivyopokewa katika swaheeh Muslim, kwa sababu hairuhusiwi kumuua Jinni bila ya haki, kama ambavyo ni haraam kumuuwa binadaam bila ya haki. Kufanya uovu ni haraam katika hali zote; hata kama ni kaafir.

Ikiwa Jinni atasikiza waadhi basi ni bora na ni vizuri, laa sivyo, basi twabibu na amkemee Jinni huyo, na amtishe, amlaani, na amtukane, kama ilivyotajwa katika swaheh Muslim, hadeeth ya Abud-Dardaa' aliyesema: 'Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisimama tukamsikia akisema *"Audhubillaahi Minka" (Najilinda kwa Allaah kutokana na wewe) kisha akasema "al-anuka bi laati Llah" (nakulaani kwa laana ya Allaah) mara tatu na akafikisha mkono wake kama kwamba ataka kuchukuwa kitu. Alipomaliza kuomba tukasema: Ewe Mtume wa Allaah tumekusikia ukisema kitu hatujawahi kukusikia ukisema kabla, na tumekuona ukifikisha mkono wako (kuunyosha). Akasema: "Adui wa Allaah Iblees alikuja na rurumbi la moto ili anitupie usoni mwangu, ndipo nikasema 'Audhu bi Llahi minka,' mara tatu. Kisha nikataka kumshika, na Wallaahi lau kama isingelikuwa ni dua ya ndugu yangu Sulaymaan, ningelimfunga asubuhi hii na vijana wa watu wa Madeenah wangelimchezea."*

[Swaheeh al-jaami' No. 3108]

Hadeeth hii yaonyesha yakwamba mtu anaweza kujilinda na Allaah kutokana na Shaytaan na kumlaani kwa laana ya Alaah.

Ikiwa Jinni atafukuzwa kwa kusoma Qur'an, kulinganiwa wema na kukatazwa mabaya, na kumkemea na kumlaani, basi lengo litakuwa limepatikana. Ikiwa hili litamsababisha Jinni kuwa mgonjwa au kufa, basi mwenyewe ndiye aliyejidhulumu, na twabibu atalipwa ajra yake kwa hilo, kwa sababu kwa kulifanya hili amemuondoshea janga yule aliyedhulumiwa. Kumsaidia yule aliyedhulumiwa ni jambo lililolinganiwa katika Uislaam, kwa kadiri na uwezo wa mtu awezavyo, na ni kitendo chenye kupendekezwa (mustahaab). Katika swaheeh mbili, Al-Bara ibn 'Aazib (رضي الله عنه) alisema: "Mtume (صلي الله عليه وسلم) alituamrisha kufanya mambo saba na akatukataza kuyafanya mambo saba, alituamrisha kutembelea wagonjwa, kuhudhuria mazishi, kusema *"Yarhamuka-llaah"* (Allaah akurehemu) kwa anaye chemua, kutimiza kiapo cha mtu (ahadi) kumsaidia aliyedhulumiwa, kukubali uaalishi, na kueneza salamu. Na akatukataza (wanaume) kuvaa pete za dhahabu, kunywa kwa vyombo vya fedha na kutumia matandiko ya hariri na kuvaa nguo za Qassiy na kuvaa hariri, marembo ya hariri yenye taraza.

Kwenye as-Swaheeh imehadithiwa kutoka kwa Anas (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: *"Msaidie ndugu yako akiwa ni dhalimu au mwenye kudhulumiwa." Nikasema ewe Mtume wa Allaah (twajua vipi) kumsaidia yeye ikiwa amedhulumiwa, lakini tutamsaidia vipi ikiwa yeye ni dhalimu? Akasema* (صلي الله عليه وسلم)**:** *"Mzuwie asidhulumu. Hivyo ndivyo unavyomsaidia."*

Kumtoa Jinni vilevile ni kumpa nafuu yule aliyedhulumiwa. Katika Swaheeh Muslim, imepokewa kutoka kwa Abu Hurayrah (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: *"Yeyote atakayemuondoshea Mu'min janga katika majanga ya dunia, Allaah atamuondolea janga katika majanga ya siku ya Kufufuliwa. Yeyote atakayefanya wepesi kwa mwenye shida, Allaah atamfanyia wepesi katika dunia na Akhera. Yeyote atakayemsitiri Muislamu, Allaah atamsitiri katika dunia na Akhera. Allaah atamsaidia mtu ikiwa mtu atamsaidia mwenzake."*

Vilevile imepokewa katika swaheeh Muslim kutoka kwa Jaabir Ibn Abdullah kuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) aliulizwa kuhusu Ruqyah akasema: *"Yeyote miongoni mwenu awezayekumfaa ndugu yake naafanye hivyo."*

Hadeeth hizi zote zamuhimiza twabibu kumsaidia ndugu yake, lakini twabibu na asijisahau katika kuuliza masuali yasiyokuwa na haja, au kuingia katika mazungumzo mengi na Jinni, isipokuwa yale yatakayotosheleza kukidhi haja, hii ni kwa sababu zifuatazo:

1 Kuuliza masuali mengi humpelekea twabibu kuingia katika mtego wa Shaytaan na aanze kujazwa na kujisifu na kiburi.

2 Katika masuali haya, Jinni huenda akagundua kuwa twabibu hana ujuzi kwahivyo aweza akawa msumbufu na akakataa kutoka.

3 Kifafa cha mda mrefu chaweza kumdhoofisha mgonjwa kimwili baada ya kupata fahamu zake.

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 4)

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

Ikiwa majaribio haya ya kumkinaisha Jinni kutoka hayakufaulu, twabibu atakikaniwa asome aya zifuatazo ambazo zitakuwa na athari kwa Jinni na kumuadhibu na kumtesa. Qur'an yote ni Tiba na ni Baraka, Allaah amesema: "**Na tunateremsha katika Qur'an (hayo mafundisho yake) ambayo ni ponyo (poza la nyoyo) na Rehema kwa wanaoamini..**" [Al-Israa' 17: 82].

AYA ZENYE KUMUADHIBU JINNI NI:

1. **Al-Faatihah**.
2. **Aayat Al-Kursiy**.
3. **Al-Nisa' (167-173)**.
4. **Al-Maa'idah (33-34)**.
5. **Al-An'aam (93)**.
6. **Al-A'raaf (44-51)**.
7. **Al-Anfaal** (12-13).
8. **Al-Tawbah** (7).
9. **Ibraheem (15-17)**.
10. **Al-Hijr (16-18)**.
11. **Al-Isra' (110-111)**.
12. **Al- Anbiya (70)**.
13. **Al-Dukhaan (43-52)**.
14. **Al-Ahqaaf (29-34)**.
15. **Al-Hajj (19-22)**.
16. **Maryam (68-72)**.
17. **Al-Mulk (5-11)**

Ikiwa Jinni bado ni msumbufu na ashindana na kukataa kutoka, basi twabibu aweza kutumia njia zifuatazo:

MATONE YA UDI WA KIHINDI

Matone ya udi wa Kihindi ndani ya pua yaweza kutumiwa kumuudhi Jinni msumbufu. Mgonjwa afaa kutia ndani ya pua, ili udi ufike moja kwa moja ndani ya ubongo wake, mahali alipo huyo Jinni, na ataudhika mno kwa huo udi, kiasi cha kwamba hatoweza kuvumilia na ataharakisha kukimbia, au atazungumza na twabibu na kuahidi kutoka na asirudi tena. Sunnah yataja uzuri wa udi wa Kihindi kama katika hadeeth iliyopokewa na Al-Bukhari (رحمه الله) katika saheeh yake:

Imehadithiwa kuwa Umm Qays bint Mihsan (رضي الله عنها) alisema: "Nimemsikia Mtume (صلي الله عليه وسلم) akisema: '**Tumieni Udi huu wa Kihindi kwani una tiba saba, waweza kutia kama matone ndani ya pua kwa maradhi ya koo au kutia pambizoni mwa kinywa kwa ajili ya (pleurisy) kifua kikuu.**" (huu ni ugonjwa wa kukohoa kwa nguvu na unaosababisha mapafu kufanya maji na kufura)

At-Timidhee alipokea hadeeth marfoo' kutoka kwa Ibn 'Abbaas (رضي الله عنه): **"Kitu bora ambacho mwaweza kutumia kwa Tiba ni matone yanayotiwa puani."**

Al-Bukhari (رحمه الله) ameita miongoni mwa milango kwenye kitabu chake "Mlango wa kutumia matone (ya udi wa kihindi) ndani ya pua."

Abu Bakr Ibn al-'Arabi (رحمه الله) alisema yakwamba udi ni sampuli mbili -udi wa Kihindi ambao ni mweusi na udi wa baharini ambao ni mweupe. Udi wa Kihindi ni moto zaidi na ndio zingatio letu katika makala haya kwa sababu udi huo ndiwo unaomuudhi Jinni.

Al-Haafidh Ibn Hajar (رحمه الله) akaeleza kuhusu maneno yalio juu, "Kwani ndani yake mna tiba ya magonjwa saba." Mawili pekee katika saba ndiyo yaliotajwa, aidha Mtume (صلي الله عليه وسلم) alitaja yote saba lakini mwenye kuhadithia amefupisha, au alitaja mawili pekee kwa sababu hayo ndiyo yaliokuwa yakijulikana wakati huo. Madaktari wametaja matumizi yake zaidi ya namna saba na wafasiri wametoa maoni kuwa saba yalijulikana ki-wahyi na mengine yalijulikana katika uzoefu wa utwabibu.

Ibn Hajar (رحمه الله) alisema: "Yawezekana kuwa saba yamaanisha sampuli mbali mbali za tiba kwa udi huo, kwani yaweza kutumiwa kama manukato, kinywaji, gundi, dawa ya kukanda misuli, kufukiza, kutia puani au ludood (dawa inayotiwa pambizoni mwa kinywa). Manukato ni kila kitokamanacho na krimu na mchanganyiko wa mafuta na hupakwa mwilini. Kinywaji yamaanisha yakwamba husagwa ikawa unga ikachanganywa na asali au maji au vitu vyengine. Hivyo hiyo katika hali ya fomentations. Katika hali ya matone yatiwayo ndani ya pua yasagwa na kuchanganywa na mafuta ya zeti (olive oil), na mchanganyiko huo, matone yake hutiwa puani. Na hivyo pia katika hali ya fututa (dawa ya kuchua). Na kinachomaanishwa kuhusu kufukiza yaeleweka.

Matumizi haya yote yana faida katika kutibu maradhi mbali mbali. Hili halifai kugutusha watu kwa sababu Mtume (صلي الله عليه وسلم) alikuwa ni mbainifu katika maneno mafupi yenye maana nyingi.

UTAYATIAJE MATONE YA UDI WA KIHINDI NDANI YA PUA?

ENDELEA KATIKA MAKALA YAJAYO

NENO LA BUSARA

Amesema Ibn Mas'ud

(رضي الله عنه)

"ANAEKUJILIA NA HAKKI, IKUBALI HAKKI ALOKUJA NAYO HATA KAMA NI MTU WA MBALI (SI WA KARIBU YAKO) UNAEMCHUKIA. NA ATAKAEKUJILIA NA BAATIL MRUDISHE NAYO (IKATAE) HATA KAMA NI KIPENZI CHAKO WA KARIBU."

Swifatus-Swafwa

Abul-Faraj Ibn al-Jawzee (رحمه الله)